***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania……!***

***Nidhamu, Haki, Weledi na Uadilifu…Ndiyo Msingi wa Mafanikio Yetu!***

Napenda kuanza hotuba hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye katujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki katika Mkutano huu wa Maafisa Waandamizi wa Jeshi la Polisi nchini. Pamoja na mambo mengine, lengo la mkutano huu ni kuweka mikakati ya kuimarisha amani, utulivu na usalama wakati wa Kampeni, wakati wa Uchaguzi na baada ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani 2025. Aidha, napenda kutumia nafasi hii kuwafikishia salamu za dhati kutoka kwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu. Mheshimiwa Rais alipokea na kuridhia ombi lenu la kuwa Mgeni Rasmi kufungua Mkutano huu. Hata hivyo, kutokana na majukumu mengine ya kitaifa aliyonayo, amenipa heshima kubwa nimwakilishe. Mheshimiwa Rais anawapongeza kwa moyo wenu wa kujituma, nidhamu na weledi katika kulinda amani na mshikamano wa Taifa letu. Anatambua mchango mkubwa mnaoutoa usiku na mchana, iwe mvua ama jua, ili kuhakikisha Watanzania wanaendelea kuishi kwa utulivu na kuendeleza shughuli zao za kujenga uchumi wa Taifa. Nami naungana naye kutoa shukrani za dhati kwa uongozi mzima wa Wizara, Mkuu wa Jeshi la Polisi, maafisa na askari wote. Kazi mnayoifanya si ya kawaida, bali ni kazi ya ujasiri, uzalendo na upendo wa kweli kwa Taifa letu. Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Dola ndivyo vinavyolinda heshima ya bendera yetu na kuhakikisha kuwa Tanzania inaendelea kuwa Taifa huru na kung’ara kama kisiwa cha amani.

***Ndugu viongozi na washiriki wa Mkutano huu;***

Kwa mujibu wa Kifungu cha 5 (1) (a – f) cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi Sura ya 322 Marejeo ya 2023, wajibu wa Jeshi la Polisi umeelezwa kuwa ni pamoja na: kulinda amani; kusimamia sheria; kubaini na kuzuia uhalifu; kukamata na kulinda watuhumiwa wa uhalifu; ulinzi wa raia na mali zao; na majukumu mengine kama itakavyoelekezwa. Kama ilivyobainishwa katika kifungu hicho, ulinzi wa amani ni moja ya majukumu ya msingi ya Jeshi la Polisi. Kwa ajili hiyo, napenda kulipongeza Jeshi la Polisi nchini, kwa kuandaa Mkutano huu wenye kaulimbiu isemayo ***"Amani, Utulivu na Usalama Kabla, Wakati na Baada ya Uchaguzi Mkuu 2025 ni Jukumu letu Sote".*** Kama ilivyokuwa katika chaguzi zilizopita, Jeshi letu la Polisi linao wajibu wa kuhakikisha amani, utulivu na usalama katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu pia, kwa kuchukua hatua za kisheria na kwa kutumia mamlaka yake kwa mujibu wa sheria, kukabiliana na viashiria vyote vya uvunjifu wa amani wakati wote. Kwa ajili hiyo, napenda kutoa wito kwa Jeshi la Polisi, wananchi na wadau wengine wa uchaguzi kuzingatia yafuatayo:

**Kwanza,** ni kuimarisha Ushirikiano na wadau wote wa Shughuli za Uchaguzi. Jeshi la Polisi lina wajibu wa kuhakikisha amani, utulivu na usalama wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani. Uchaguzi huu unahusisha wadau wengi, wakiwemo wananchi wenye itikadi mbalimbali za kisiasa, wagombea wa nafasi mbalimbali, Tume Huru ya Uchaguzi, viongozi wa dini na mila, wanaharakati, pamoja na waangalizi wa

uchaguzi wa ndani na nje ya nchi. Ili kufanikisha jukumu hili, ni muhimu Jeshi la Polisi kuimarisha ushirikiano wa karibu na wadau wote wa uchaguzi. Hatua hii itasaidia kuhakikisha kila mdau anatendewa haki, na kuondoa tofauti zinazoweza kusababisha migongano au machafuko. Baadhi ya maeneo muhimu ya ushirikiano ni pamoja na: kuhakikisha mikutano ya kampeni inafanyika kwenye maeneo yaliyoruhusiwa na ndani ya muda uliopangwa; Kuzuia maandamano yasiyo na kibali ambayo yanaweza kusababisha vurugu, uharibifu wa mali, majeruhi au vifo; Kuimarisha ulinzi wa wagombea na viongozi wa vyama vya kisiasa, bila kujali vyama vyao au itikadi zao; na Kudhibiti misongamano mikubwa ya watu ili kuhakikisha shughuli nyingine za kijamii na kiuchumi zinaendelea bila usumbufu. Kwa kufanya hivyo, Jeshi la Polisi litachangia kwa kiasi kikubwa katika kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa amani, haki na utulivu, huku likilinda masilahi ya Taifa kwa ujumla.

**Pili,** ni kusimamia utekelezaji wa sheria ya uchaguzi na sheria nyingine za nchi: Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge, na Madiwani unafanyika kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977, Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya Mwaka 2024 na Sheria nyingine za nchi. Ukosefu wa amani, utulivu na usalama unaweza kusababishwa na kutozingatia au kutosimamia ipasavyo sheria ya uchaguzi. Mathalan, Sheria ya Uchaguzi imeweka masharti mbalimbali yanayopaswa kuzingatiwa ili kuwa na uchaguzi huru na wa haki, kuanzia uandikishaji wa wapiga kura, uteuzi wa wagombea wa nafasi mbalimbali, kampeni za uchaguzi, utaratibu wa kupiga na kuhesabu kura, makosa ya uchaguzi na utaratibu wa kupinga matokeo ya uchaguzi. Hivyo, ni wajibu wa Jeshi la Polisi na wadau wengine wa uchaguzi, kuielewa vizuri sheria hii na kusimamia utekelezaji wake, ili kuepuka kuonea watu na kuvuruga uchaguzi. Napenda kutoa wito pia kwa wananchi na viongozi wa vyama vya siasa kuepuka kujichukulia sheria mkononi pale wanapoona ukiukwaji wa sheria za uchaguzi, na badala yake watoe taarifa kwenye vyombo vya sheria kwa hatua stahiki.

**Tatu,** Jeshi la Polisi lishirikiane kwa karibu na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) pamoja na taasisi nyingine za Serikali ili kujiandaa vyema kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kufuatilia taarifa mbalimbali zenye mlengo wa uchochezi, zinazotolewa kupitia mitandao ya kijamii na vyombo vingine vya habari. Kama mnavyofahamu, mitandao ya kijamii hutumika kusambaza sera na Ilani za vyama vya siasa pamoja na wagombea wao. Hata hivyo, mitandao hii pia inaweza kutumiwa kusambaza taarifa za uongo, kueneza uchochezi na upotoshaji wa makusudi, jambo ambalo linaweza kusababisha taharuki na mgawanyiko katika jamii. Zaidi ya hayo, kwa kutumia teknolojia za akili bandia (*Artificial Intelligence - AI*), baadhi ya watu wanaweza kusambaza picha au video za uongo za wagombea wa vyama vya siasa, jambo linaloweza kuleta madhara makubwa kwa amani na utulivu wa jamii. Kwa ajili hiyo, Jeshi la Polisi linapaswa kujiandaa kikamilifu kufanya doria ya mtandao (*cyber surveillance*) ili kubaini na kuchambua machapisho, picha, na video zenye viashiria vya uvunjifu wa sheria, na kuchukua hatua za kisheria kwa haraka.

***Ndugu viongozi na washiriki wa Mkutano huu;***

**Nne,** Jeshi la Polisi lishirikiane kwa karibu na wadau wengine wa uchaguzi, ikiwemo TAKUKURU na vyombo vingine vya usalama, ili kudhibiti vitendo vya Rushwa katika

kipindi hiki cha uchaguzi. Wananchi wanatakiwa kuchagua viongozi kwa kuzingatia Ilani za vyama vya siasa pamoja na uwezo halisi wa kiuongozi wa wagombea husika. Viongozi waliopatikana kwa vitendo vya rushwa hawana uchungu wa rasilimali za nchi, jambo linaloweza kuathiri maendeleo ya wananchi kwa ujumla. Hivyo, Jeshi la Polisi lijizatiti ipasavyo kwa kushirikiana na TAKUKURU katika kukabiliana na vitendo vya rushwa wakati wa Uchaguzi Mkuu. Aidha, napenda kutoa wito kwa wananchi na wadau wote wa uchaguzi kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwa TAKUKURU, ili hatua madhubuti zichukuliwe kwa haraka na kuhakikisha kuwa wananchi wanachagua viongozi bora kwa hiari yao, si kwa kununuliwa.

**Tano,** vilevile ni muhimu Jeshi la Polisi likijumuisha Polisi Jamii lishirikiane kwa karibu na TAMISEMI katika kusimamia usalama, hasa katika ngazi za Kata, Shehia, Vijiji na Mitaa. Viongozi wa ngazi hizo wana jukumu la kudumisha amani na utulivu katika maeneo yao. Hivyo, ushirikiano mzuri kati ya Jeshi la Polisi, Polisi Jamii na viongozi hao utasaidia kuzuia migogoro na kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa utulivu na amani. Nawahimiza Jeshi la Polisi kuimarisha mahusiano na viongozi katika ngazi hizo ili kuwezesha ushirikiano madhubuti wa kudumisha amani katika Taifa letu, hasa wakati huu wa uchaguzi mkuu.

**Sita,** tunapoelekea kwenye uchaguzi mkuu ni muhimu kuendelea kuwajengea uwezo maafisa na askari kwa kuwapatia mafunzo ya utayari, uadilifu, na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao. Napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) kwa kuendelea kuhakikisha kwamba askari wa Jeshi la Polisi wanapata mafunzo ya kitaalam ya kuwajengea uwezo na utayari. Hatua hii ni muhimu ili kuwawezesha askari kuwa na uelewa mzuri, nidhamu, na ufanisi unaotakiwa ili kutekeleza majukumu yao kwa weledi na uadilifu mkubwa katika kufanikisha zoezi la uchaguzi mkuu.

**Saba,** Kama wote tunavyofahamu, Serikali imetumia fedha nyingi kununua magari, boti, pikipiki na inakamilisha mchakato wa kununua helikopta zaidi za Jeshi la Polisi, pamoja na vitendea kazi vingine vitakavyotumika katika kuhakikisha zoezi la uchaguzi mkuu linafanyika katika hali ya utulivu na amani. Napenda kutumia fursa hii kutoa wito kwa wote mtakaokabidhiwa rasilimali hizo kuhakikisha zinatuzwa vizuri, na zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa tu.

***Ndugu viongozi na washiriki wa Mkutano huu;***
Mwisho, naomba nimalizie hotuba yangu kwa kuwashukuru kwa mara nyingine kwa mapokezi mazuri, ikiwemo gwaride la kiwango. Ninautakia mkutano huu mafanikio makubwa. Baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, sasa ninayo heshima kutamka rasmi kuwa, ***"Mkutano Mkuu wa Mwaka 2025 wa Maafisa Waandamizi wa Jeshi la Polisi,*** umefunguliwa rasmi."

**Nidhamu, Haki, Weledi na Uadilifu…Ndiyo Msingi wa Mafanikio Yetu!**

**ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA.**